# JARIDA LA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

*Wizara ya Furaha*

Toleo Maalum la: 19 | 28 Juni, 2021 | www.habari.go.tz

# MASHINDANO YA NGOMA UMISSETA 2021 YASISIMUA



Wizara HabariTz Wizara_habaritz Wizara_HabariTZ

# YALIYOJIRI KATIKA WA MASHINDANO YA MICHEZO YA UMISSETA

## 28 Juni, 2021

**KAULIMBIU:** "MICHEZO SANAA NA TAALUMA KWA MAENDELEO YA UCHUMI WA VIWANDA"

# NUKUU YA MRATIBU WA MPIRA WA WAVU UMISSETA 2021 SOMO KIMWAGA

Mchezo wa wavu ndiyo mchezo pekee wenye mashabiki wengi ukiondoa soka kwenye mashindano haya ya UMISSETA 2021 yanayoendelea Mjini Mtwara.

Tulijipanga vizuri zaidi mwaka huu, napenda kukujulisha kuwa timu zangu zinaanza mtanange wa robo fainali kesho ila leo Juni 28, 2021 wachezaji wa timu zote tumewapumzisha hatufanyi michezo yoyote lakini viwanja vyote vya mchezo huu vimejaa wachezaji ambao ni washabiki na wapenzi wa mchezo huu.



Wamehamasika na wamejitokeza kwa wingi kucheza pia kufanya mazoezi na kujifunza mchezo huu utadhani mechi za mashindano zinaendelea!

Hii inatokana na kazi kubwa ya kuufanya mchezo huu uchezwe zaidi kwa kuwa na mikakati ya kuwafundisha makocha,waamuzi na walimu kuanzia ngazi ya Shule za Msingi na Sekondari, pia kutoa mafunzo kwenye vyama vya michezo.

Natumia nafasi hii kumpongeza Kocha wa Timu ya Mkoa wa Mtwara Wanawake kwa kuwa na program nzuri ya mazoezi katika kipindi chote cha mwaka.

Nawashauri wanamichezo wote tukimaliza michezo ya UMISSETA ya mwaka huu iwe mwanzo wa kuendelea kufanya mazoezi zaidi ili kuinua kiwango cha mchezo huu pendwa hapa nchini.

**SOMO KIMWAGA**

**Mratibu wa Mpira wa Wavu – UMISSETA 2021**

# ARUSHA, GEITA MABINGWA MCHEZO WA KURUKA JUU UMISSETA 2021

Mikoa ya Arusha na Geita imeongoza kwenye mchezo wa kuruka juu katika Mashindano ya Taaluma na Michezo kwa Shule za Sekondari (UMISSETA) kwenye fainali zilizofanyika leo Juni 28, 2021 mjini Mtwara.

Msemaji wa UMISSETA 2021, John Mapepele amesema Kanjori Sambeke kutoka Arusha ameibuka kuwa mshindi wa kwanza baada ya kuruka urefu wa mita 1 na sentimita 78 akifuatiwa na Erasto Mwaipopo kutoka mkoa wa Mbeya aliyeruka urefu wa mita 1 na sentimita 76 wakati nafasi ya tatu imechukuliwa na Silinde Marwa kutoka Mkoa wa Mara aliyeruka urefu wa mita 1 na sentimita 74.

Kwa upande wa wasichana Witiness Ibrahimu kutoka Mkoa wa Geita ndiye Mshindi wa kwanza kwa kuruka umbali wa mita 1 na sentimita 44. akifuatiwa na Naima Mohamed kutoka Shinyanga aliyeruka juu kwa mita1na sentimita 43 ambapo nafasi ya tatu ilichukuliwa na Karolina Erasto kutoka Singida aliyeruka urefu wa mita 1 na sentimita 43.

Ikumbukwe kuwa Witiness ndiye mshindi wa kwanza UMISSETA 2021 kwenye mchezo wa kuruka miruko mitatu ambapo alishinda kwa kuruka umbali wa mita 9 na sentimita 67 katika mchezo wa Juni 27,2021. Hii unaufanya mkoa wa Geita kuwa mshindi wa kwanza katika michezo miwili;mchezo  wa mruko mitatu na kuruka juu kwa upande wa wanawake katika mashindano haya.

# MWANAMICHEZO WA SIKU

MSHIRIKI KANJORI SAMBEKE KUTOKA ARUSHA ALIYESHIRIKI MCHEZO WA KURUKA JUU NDIO MWANAMICHEZO WA SIKU.





Namshukuru Mungu kwa kuniumba mrefu, nitaendelea kutumia umbo langu alilonijalia Mwenyezi Mungu kufanya mazoezi zaidi ili niiwakilishe nchi yangu katika mashindano ya mchezo huu kimataifa.

Huu ni mwaka wangu wa kwanza kushiriki mashindano ya UMISSETA nafurahi nimeibuka  mshindi wa kwanza baada ya kuruka urefu wa mita 1 na sentimita 78 na kuwashinda wenzangu wote.

**KANJORI SAMBEKE**

**Mshindi wa kwanza Mchezo wa Kuruka Juu,**
**UMISSETA 2021 – Mkoa wa Arusha**

# MPIRA WA PETE

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA PETE KWA WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 28, 2021. TIMU ZA MIKOA YA IRINGA 7 (WENYE KIJANI NA BLUU NYEUSI) NA SONGWE 44 (WENYE NYEUSI NA PINKI).





# MPIRA WA PETE

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA PETE KWA WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 28, 2021. TIMU ZA MIKOA YA KATAVI 24 (WENYE NYEUPE) NA SINGIDA 31 (WENYE BLUU NYEUSI).






# MPIRA WA PETE

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA PETE KWA WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 28, 2021. TIMU ZA MIKOA YA MTWARA 14 (WENYE NYEUPE NA BLUU NYEUSI) NA KAGERA 34 (WENYE NJANO NA BLUU).






# MPIRA WA PETE

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA PETE YAMEENDELEA LEO, JUNI 27, 2021. TIMU ZA MIKOA YA SHINYANGA 33 (WENYE PINKI NA NYEUPE) NA RUVUMA 22 (WENYE BLUU NYEUSI NA RANGI YA CHUNGWA).






# MPIRA WA KIKAPU WASICHANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA KIKAPU KWA WASICHANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 28, 2021. TIMU ZA MIKOA YA LINDI 18 (WENYE NYEKUNDU) NA SIMIYU 6 (WENYE ZAMBARAU).





# MPIRA WA KIKAPU WAVULANA

MASHINDANO YA UMISSETA MPIRA WA KIKAPU KWA WAVULANA YAMEENDELEA LEO, JUNI 28, 2021. TIMU ZA MIKOA YA DAR ES SALAAM 60 (WENYE NJANO) NA RUKWA 10 (WENYE KIJANI).






# MPIRA WA WAVU

## MASHINDANO YA MPIRA WA WAVU
## KATI YA MAKOCHA
## NA WAAMUZI.





# MASHINDANO YA RIADHA
# KURUKA JUU – WAVULANA

**KANJORI SAMBEKE KUTOKA ARUSHA AMEIBUKA KUWA MSHINDI WA KWANZA BAADA YA KURUKA UREFU WA MITA 1 NA SENTIMITA 78.**



# MASHINDANO YA RIADHA
# KURUKA JUU – WASICHANA

**WITINESS IBRAHIMU KUTOKA MKOA WA GEITA NDIYE MSHINDI WA KWANZA KWA KURUKA UMBALI WA MITA 1 NA SENTIMITA 44.**



# SANAA ZA NDANI
# NGOMA ZA ASILI

MASHINDANO YA UMISSETA UPANDE WA SANAA ZA NDANI (NGOMA ZA ASILI) YAMEENDELEA LEO, JUNI 28, 2021. MIKOA ILIYOSHIRIKI LEO NI SONGWE, TABORA, NJOMBE, LINDI, DAR ES SALAAM NA ZANZIBAR.



SONGWE




TABORA



NJOMBE



LINDI



DAR ES SALAAM



ZANZIBAR

UMITASHUMTA | UMISSETA 2021

# #MwakaWaVipaji

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
S.L.P 25, 40470 DODOMA, TANZANIA